JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017

[*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*]

Idara ya Kamati za Bunge
S.L.P. 941,
DODOMA

07 Februari, 2017

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA 2
1:0 MAELEZO YA JUMLA 2
1.1 Utangulizi 2
1.2 Wajumbe wa Kamati 2
1.3 Majukumu ya Kamati 3
SEHEMU YA PILI 5
2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI 5
2.1 Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 5
2.2 Sekta ya Uchukuzi 5
2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA 5
2.2.2 Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) 9
2.2.3 Ujenzi wa Reli ya Kati 9
2.2.4 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA 12
2.2.5 Shirika la Ndege Tanzania-ATCL 14
2.2.6 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania – TMA 15
2.2.7 Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini - SUMATRA 15
2.3 Sekta ya Ujenzi 16
2.3.1 Wakala wa Barabara Tanzania- TANROAD 16
2.4 Sekta ya Mawasiliano 20
2.4.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) 20
2.4.2 Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta 21

SEHEMU YA TATU 25
3.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI 25
3.1 Bajeti ya Miundombinu 25
3.2 Sekta ya Uchukuzi 25
3.3 Sekta ya Ujenzi 36
3.4 Sekta ya Mawasiliano 39
SEHEMU YA NNE 42
4.0 HITIMISHO 42
4.1 Shukrani 42
4.2 Hoja 43

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KWA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017

SEHEMU YA KWANZA

1:0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017.

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa Taarifa hii umegawanyika katika maeneo makubwa manne yafuatayo:-

a. Sehemu ya I- Maelezo ya Jumla (Utangulizi);
b. Sehemu ya II- Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati;
c. Sehemu ya III- Maoni, Mapendekezo na Ushauri wa Kamati; na
d. Sehemu ya IV- Hitimisho

1.2 Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe .Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb -Mjumbe
4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb ,,
5. Mhe. Mizar Bakari Haji, Mb ,,
6. Mhe. James Francis Mbatia, Mb ,,
7. Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb ,,

8. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb ,,
9. Mhe. Saul Henry Amon, Mb ,,
10. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb ,,
11. Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb ,,
12. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb ,,
13. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb ,,
14. Mhe.Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb ,,
15. Mhe. Mary Deo Muro, Mb ,,
16. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb ,,
17. Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassym, Mb ,,
18. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb ,,
19. Mhe. Dua William Nkurua, Mb ,,
20. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb ,,
21. Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb ,,
22. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb ,,
23. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb ,,
24. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb ,,
25. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb ,,
26. Mhe. Charles Kitwanga, Mb ,,
27. Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka, Mb ,,

1.3 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 6(8), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imepewa jukumu la kuisimamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Katika kusimamia Wizara hiyo, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Aprili, 2016 imeainisha majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoisimamia;
b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara husika;

c) Kufuatilia Utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inayoisimamia;

d) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara husika; na

e) Kufuatilia Utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa Mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

1.4 Shughuli zilizofanyika kwa Kipindi cha Mwaka 2016/2017

Mheshimiwa Spika, ***kiambatisho namba 1*** kinaonesha mchanganuo wa majukumu yote yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017. Aidha, jedwali hilo limebainisha shughuli zilizofanyika, njia mbali mbali zilizotumika ikiwepo vikao, ziara na semina.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Mapendekezo na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto kubwa ni Serikali kutokupeleka fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeidhinishiwa shilingi trilioni 4.2 (4,229,408,685,900.00) ambayo ni sawa na asilimia 16.7 ya Bajeti yote ya Serikali. Kamati imebaini kuwa mwenendo wa Bajeti hii si mzuri kwani taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa nusu ya mwaka wa fedha (Julai-Desemba 2016) inaonesha miradi mingi bado haijapatiwa fedha. Fedha zilizopelekwa ni Ujenzi asilimia 38.3; Uchukuzi asilimia 34.3; na Mawasiliano asilimia 24.

2.2 Sekta ya Uchukuzi

2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA zikiwemo:-

a. Kuzorota kwa huduma za reli nchini jambo linalosababisha usafirishaji wa mizigo kutegemea barabara pekee;

b. Uwezo mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli kubwa na kina kifupi katika bandari ya Dar es Salaam pamoja naTanga;

c. Uchakavu wa miundombinu ya bandari nchini;

d. Uwepo wa bandari bubu na ushindani wa Bandari zingine kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa-Kenya na Durban-Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi kabisa na hali ya bandari nchini kwani shehena zimeendelea kushuka ukilinganisha na mwaka uliopita. Mfano; katika Bandari ya Dar es Salaam katika mwaka 2014/15 kulikuwa na upungufu wa asilimia 5.2 ukilinganisha na mwaka 2015/16 na katika kipindi cha nusu mwaka 2015/16 na 2016/17 kumekuwa na upungufu wa shehena asilimia 0.1. Bandari ambazo zimeathirika na kushuka kwa shehena ni pamoja na Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mwanza, Bandari ya Kigoma na Bandari ya Itungi-Kyela.

a) Bandari ya Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bandari ya Dar es Salaam; hii ndio bandari mama na bandari kubwa kuliko zote Tanzania ambayo inahudumia nchi jirani ambazo hazina bandari kama vile Rwanda, Burundi, DR Congo, Uganda, Zambia na Malawi. Hata hivyo, pamoja na kuwa katika nafasi nzuri ya kijiografia bado bandari hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za miundombinu inayounganisha bandari kama vile reli na barabara na kutokuwepo kwa maegesho kwa ajili ya magari yanayoenda kupakia mizigo bandarini hivyo kuathiri uondoshaji wa mizigo kutoka bandarini. Kwa ujumla changamoto hizi zinasababisha nchi kupoteza wateja wengi waliokuwa wakitumia bandari ya Dar es Salaam na kwa sasa kuhamia katika bandari zingine shindani za Mombasa- Kenya, Beira- Msumbiji, Durban- Afrika Kusini na Walvis Bay-Namibia ambazo zimeweka mazingira rafiki na wafanyabiashara na kuvutia wengi kukimbilia huko.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa bandari ya Dar es Salaam, ni muda sasa tangu kumekuwepo mipango mbalimbali ya

kuboresha na kuendeleza bandari hii ili iweze kuhudumia meli kubwa na kuweza kuhudumia ongezeko kubwa la shehena linalotarajiwa kwa miaka ijayo. Kamati imejulishwa kuwa mipango hiyo imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

i) Kuhusu uboreshaji na uongezaji wa kina katika gati namba 1 hadi 7 na ujenzi wa gati mpya yakushushia magari eneo la Gerezani Creek. Zabuni kwa hatua ya pili na ya mwisho kwa ajili ya kupata mkandarasi wa kazi za ujenzi zimepelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuridhia ili zitolewe kwa makampuni na wakandarasi yaliopita katika hatua ya kwanza ya mchujo. Zabuni zilitolewa mwezi Februari 2016 na kufungwa Julai 2016. Kampuni ya M/S Inros Lackner Ag ya Ujerumani ndio iliyoteuliwa kuwa msimamizi wa kazi ya ujenzi;

ii) Kuhusu uchimbaji wa lango la kuingilia meli na sehemu ya kugeuzia hadi kina cha mita 15.5 pamoja na kupanua lango. Mkataba na Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya Upembuzi yakinifu ulisainiwa mwezi Disemba 2015 na kazi zilinza tarehe 20 Januari 2016 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Februari 2017;

iii) Kuhusu ujenzi wa gati namba 13 na 14, baada ya Serikali kushauriana na wafadhili wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam mwezi Oktoba 2015, ilikubalika kujumuisha magati yote ya bandari kwenye mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo unatarajiwa kuanza rasmi mwaka 2018 baada ya kukamilika kwa uhamishaji wa gati la mafuta la *Kurasini Oil Jet* (KOJ) na mabomba yake.

b) Bandari ya Mwanza

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto zilizotajwa awali zinazorotesha bandari nchini, bandari ya Mwanza inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i) Ujenzi wa vituo vya kuegesha meli ambavyo ni vya watu binafsi na baadhi siyo rasmi. Vituo kadhaa vimejengwa karibu sana na bandari ambapo

pamoja na kuinyima mapato Serikali pia vinatishia usalama na utaratibu wa uendeshaji wa meli katika Maziwa;

ii) Mgogoro kati ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Bandari Mwanza kuhusu mipaka ya bandari pamoja na tozo mbalimbali za ushuru kwa magari yanayoingia na kutoka bandarini jambo linalosababisha gharama kwa wafanyabiashara na hivyo kuona usumbufu na kuamua kutumia bandari nyingine; na

iii) Ushindani mkubwa kutoka kwa bandari bubu pamoja na kuharibika mara kwa mara kwa meli ya MV Serengeti na MV Victoria ambazo zimekuwa ndiyo tegemeo kubwa la usafiri wa mwambao wa Ziwa Victoria.

c) Bandari ya Tanga

Mheshimiwa Spika, licha ya changamoto mbalimbali zinazoikabili bandari ya Tanga, bandari hii imekuwa ikijiendesha kwa hasara tangu mwaka 2013 hivyo kuwa mzigo kwa Mamlaka ya Bandari nchini. Pamoja na kujiendesha kwa hasara, miradi mbalimbali ya maendeleo imekuwa ikiendelea ikitekelezwa kama vile ujenzi wa bandari ya Mwambani, kuimarisha gati namba mbili (2) na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kati ya Uganda na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa bandari ya Mwambani-Tanga, baada ya upembuzi yakinifu kukamilika Agosti 2012 hatua zilizofikiwa ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kumilikishwa eneo la ardhi lenye ukubwa wa hekta 92 ambalo ni kwa awamu ya kwanza pamoja na kulipa fidia kwa Halmashauri ya jiji la Tanga kiasi cha shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo la mradi.Taratibu za umilikishwaji wa eneo jingine la ardhi lenye hekta 82 zinaendelea. Hata hivyo, Kamati ilishangazwa kuona kuwa jiwe la msingi liliwekwa mnamo mwaka 1975 hata

hivyo wananchi waliendelea kujenga na kuishi katika eneo hilo na baadae kudai kulipwa fidia.

2.2.2 Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa imekuwa ni uchakavu wa Meli kutokana na kutokufanyiwa matengenezo makubwa kwa wakati na hivyo kusababisha gharama kubwa za uendeshaji. Mfano, MV Butiama ambayo haifanyi kazi tangu mwaka 2010, MV Victoria nayo haifanyi kazi toka mwaka 2014 na MV Liemba ambayo inafanya kazi lakini kwa kusuasua. Katika kutatua changamoto hizo, mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga **shilingi bilioni 50.5 (50,500,000,000)** kwa ajili ya malipo ya asilimia 50 ya ujenzi wa meli mpya ya Ziwa Victoria, ukarabati wa MV Victoria (MSCL), ukarabati wa MV Liemba na MV Butiama. Kamati imejulishwa kuwa kazi hii ipo kwenye uchambuzi wa zabuni.

2.2.3 Ujenzi wa Reli ya Kati

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* ni muhimu sana. Kamati katika hotuba yake ya mwaka wa fedha wa 2016/17 iliishauri Serikali kuwa kampuni ya reli ya Serikali ya China iliyojenga kipande cha Reli ya mfano kwa ajili ya uzinduzi pale Soga-Kibaha, kwa ubora uleule iendelee. Na kamati ilitoa angalizo la kuharakisha uamuaji na ujengaji wa reli ya kati kwa kuwa kukamilisha haraka ujenzi wa reli hiyo ndiyo faida kwa uchumi unaotokana na mizigo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa fedha za ujenzi wa reli ya kati yaani **dola 7.6 bilioni** zitatolewa kama mkopo wenye masharti nafuu na Serikali ya China kupitia China Exim bank. Na kwamba hii ilipelekea kutengwa kwa **shilingi trilioni 1** kama sehemu ya **asilimia 15** ya mchango wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo. Kwenye hotuba ya kamati tuliangaliza kuwa mzigo

unaotegemewa na Tanzania pia unategemewa na nchi jirani. Kwa maantiki hiyo kukamilisha ujenzi wa reli ya kati haraka ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ujenzi wa reli ya kati yalianza kipindi kilekile na ujenzi wa reli ya kutoka Mombasa kwenda Nairobi, nchini Kenya. Wenzetu wamemaliza, sisi bado. Maana kama mtandao wa reli wa nchi jirani utakuwa umekamilika kabla sisi hatujakamilisha reli yetu, upo uwezekano mkubwa reli yetu itakuwa ya abiria zaidi kuliko mizigo, wakati huo huo mzigo unategemewa ambao kimsingi ndiyo nguvu yetu ya kujenga reli yaani ongezeko tarajiwa la mzigo kutoka tani milioni 5 za sasa mpaka tani milioni 17 reli ikikamilika haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, Kamati tunalazimika kuelezea juhudi zinazofanywa upande mwingine wa nchi jirani kwa kuwa Tanzania si kisiwa na Miundombinu ya reli inategemea sana mzigo wa nchi jirani. Kamati inatambua kuwa yapo makubaliano ya ujenzi wa reli kutoka Mombasa, Kampala mpaka Kigali.

Mheshimiwa spika, Kamati inatambua pia kuwa kumekuwepo na makubaliano ya Tanzania na Burundi ya kuharakisha ujenzi wa tawi la kutoka Uvinza kwenda Msongati kwa ajili ya kuchukua Chuma, na pia makubaliano ya Serikali ya Tanzania na DRC Congo ya kuchukua mzigo wa kutoka Congo kupitia bandari ya Kalemi kwenye Ziwa Tanganyika. Makubaliano hayo bila shaka ni moja ya kichocheo cha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard gauge* kwa kuwa mzigo tunahakika nao. Ikiwa mtandao wa reli wa nchi jirani utakamilika kabla yetu, ni wazi tutakuwa na kazi kubwa ya kufanya ili reli ya kati iweze kuwa ya manufaa kiuchumi na maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa kwenye anga za kimataifa kila msaada unaopewa na nchi yoyote unajipambanua na nchi hiyo. Na pia Kamati inatambua kuwa kampuni ya serikali ya China ambayo ndiyo iliyojenga kipande cha reli ya mfano pale Soga Kibaha ni mali ya serikali ya China ambayo ilianzishwa mara baada ya kukamilisha ujenzi wa reli ya Tazara. Inawezekana kukawa na mapungufu ya utekelezaji wa mradi huo katika serikali ya awamu ya nne,

kutegemea nani anatazama upungufu huo na kwa nia gani, lakini ni muhimu Serikali kuhakikisha kuwa upungufu wa mtu au watu kama upo, unarekebishwa ilimradi serikali isipoteze lengo la msingi la ujenzi wa reli ya kati kupitia makubaliano yaliyopo. Serikali inaweza kusahihisha ama kurekebisha makubaliano yoyote inayotilia shaka maadam iendelee kuenzi diplomasia za kimataifa na hasa nchi zile ambazo zimejipambanua kuwa rafiki zetu awamu zote tano za serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa uchumi wa Kimataifa na mipango ya maendeleo mikubwa hasa ujenzi wa reli, viwanja vikubwa vya Ndege, ujenzi wa bandari, uchimbaji wa mafuta na gesi na miradi kama hiyo inahitaji kutokupoteza lengo maana chochote kinaweza kufanyika ili mradi tucheleweshwe katika kukamilisha miradi hiyo. Kwa mfano, pale ambapo unahifadhi ya mafuta ardhini, unaweza kuambiwa mafuta huna, utafiti uendelee; pale ambapo unatakiwa kukamisha terminal ya 3 ya uwanja wa Ndege, unaweza ukaambiwa fedha zimechelewa kupitishwa/kusainiwa/kuruhusiwa kwa hiyo subiri; pale ambapo unatakiwa ujenge gati ya bandari ya kina kirefu au bandari mpya, unaweza ukaambiwa bodi ya benki ya dunia haijapitisha mkopo mpaka kikao cha mwaka unaofuata. Ni wazi maendeleo ni vita lazima tuwe makini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya sasa uchumi wake unategemeana sana. Ukiboresha reli ya kati, maana yake pia umeboresha utoaji huduma wa Bandari ya Dar es salaam; na kwa kufanya hivyo unahatarisha bandari ya nchi zingine kwa kuwa mizigo na wateja ni walewale. Hivyo, chochote kinaweza kufanyika ili nchi ishughulikie vitu ambavyo havisaidii kujenga reli ya kati na kwa kufanya hivyo, tunabaki kusema hiki hakikufuatwa au kilifuatwa na mwisho hatujengi au tunachelewa kujenga reli yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusaini mkataba na Kampuni ya Uturuki pamoja na Ureno wa kujenga reli kutoka Dar es salaam mpaka Morogoro. Ujenzi wa reli hiyo yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia sana

kurahisisha usafiri hasa wa abiria kutoka Morogoro hadi Dar es Salaam. Ni vyema Serikali ikakamilisha pia sehemu ya reli ya kati iliyobaki na matawi yake yote.

2.2.4 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini kwani imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini licha ya changamoto kubwa zilizopo za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini. Kutopelekwa kwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati kumekuwa kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano, hadi kufikia mwezi Machi 2016, hakuna fedha zozote zilizokuwa zimetolewa kwa viwanja vya ndege isipokuwa shilingi bilioni 5 (5,000,000,000.00) tu, ambazo zilitolewa kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Kamati hairidhishwi na utolewaji wa fedha za miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege ukizingati kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inakusanya fedha nyingi zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

a) Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na nia ya kukiendeleza Kiwanja cha ndege cha Mwanza kwa kukipanua ili kiweze kukidhi mahitaji mengi ya sasa ya wakazi wa Kanda ya Ziwa hatimae kutua ndege kubwa za Kimataifa. Hata hivyo ujenzi wa mradi huu umekumbwa na changamoto ya kutotolewa kwa fedha kwa wakati hivyo kusababisha kasi ya utekelezaji wa mradi kuwa ndogo. Mfano halisi ni katika mwaka wa fedha 2015/2016, Kiwanja hiki kiliidhinishiwa **shilingi bilioni 10.7 (10,777,975,000.00)** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2016 kilikuwa kimepewa **shilingi bilioni 5 tu (5,000,000,000.00)**.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati imefarijika kuona kiwanja hiki kimetengewa **shilingi bilioni 30.1 (30,150,000,000.00)** ambapo mpaka mwezi Januari, 2017 zimetolewa **shilingi bilioni 7.6.** Ni

dhahiri kuwa fedha hizi zikitolewa kwa wakati zitaharakisha ujenzi wa kiwanja hiki.

b) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni muhimu sasa kiwanja hiki kikafanyiwa ukarabati kwani majengo na miundombinu yake yamechakaa na inahitaji ukarabati mkubwa. Kuendelea kubaki katika hali ya uchakavu ni aibu kwa nchi yetu hasa ukizingatia wageni wengi wanaotembelea nchi yetu hutumia kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la tatu la abiria *(terminal III*) katika Kiwanja hiki, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 mradi ulitengewa **shilingi bilioni 26** ambazo Kamati imejulishwa hadi Desemba 2016 fedha hizo hazikuwa zimetolewa.

c) Kiwanja cha Ndege cha Songwe

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja hiki umekuwa ukisuasua kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha jambo linalokwamisha kukamilika kwa baadhi ya maeneo yanayojengwa kama vile jengo jipya la abiria. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 5** ambazo hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 hazikuwa zimetolewa. Vivo hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu umetengewa **shilingi bilioni 7** lakini hadi kufikia Desemba 2016 hakuna fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haioni sababu za msingi za kutokumalizia Kiwanja hiki ukizingatia kuwa ili mradi huu ukamilike unahitaji fedha kiasi cha **shilingi bilioni 16.154** tu **(16,154,239,492.14).**

2.2.5 Shirika la Ndege Tanzania-ATCL

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya dhati na jitihada za kulikwamua Shirika la Ndege Tanzania- ATCL ambapo katika Bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilitenga shilingi bilioni 500 (500,000,000,000.00) kwa ajili ya ununuzi wa ndege. Mwezi Oktoba 2016 utekelezaji ulianza ambapo ndege mbili mpya aina ya Dash 8 Q400 zenye uwezo wa kubeba abiria sabini na sita (76) ambapo abiria sita (6) ni wa daraja la kibiashara ziliwasili nchini na kufanya shirika hili sasa kumiliki ndege tatu (3) ambapo moja ni aina ya Dash 8 Q300. Hata hivyo, Kamati imejulishwa kuwa Serikali inaendelea na mpango wa ununuzi wa ndege nyingine mbili zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 155.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa ATCL imeandaa orodha ya ulipaji wa baadhi ya madeni ambapo orodha imehusisha wadeni muhimu ambao hutoa huduma kwa ATCL kwa ajili ya uuzaji wa tiketi za ndege na ukusanyaji na udhibiti wa mapato. IATA Clearing House-(ukusanyaji na udhibiti wa mapato), SITA Reservation System-(huduma ya mfumo wa mauzo ya tiketi), Kampuni ya Simu Tanzania-TTCL – (huduma za mitandao ya kuunganisha vitengo mbalimbali) ni kati ya wadeni waliopewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ATCL inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha, upungufu wa wataalam hasa marubani na waaandisi ambapo wengi wao wamefikisha umri wa kustaafu, Kuchelewa kurejea katika chama cha mashirika ya ndege duniani (IATA), Kushindwa kuanza baadhi ya safari kwa wakati kwenye baadhi ya mikoa kama vile Mpanda kutokana na mapungufu katika viwanja hivyo mfano, ukosefu wa gari la zima moto. Changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi kama inavyoelekezwa katika mapendekezo ya Taarifa hii.

2.2.6 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania – TMA

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika sekta ya hali ya hewa nchini, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

a. Kukosekana kwa jengo la kudumu la Makao Makuu na Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa hivyo kuathiri taratibu za kuweka mitambo ya kisasa ya utabiri;
b. Uchache wa wataalam wa hali ya hewa ili kukidhi matakwa ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani ambapo linataka taasisi ya hali ya hewa kutumia wataalam wenye shahada ya kwanza kwa ajili ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndeg ifikapo Desemba 2016;
c. Upungufu na uchakavu wa vituo na vifaa vya kupimia hali ya hewa;
d. Mabadiliko ya mara kwa mara ya hali ya hewa Duniani yanayosababisha changamoto katika utabiri wa hali ya hewa; na
e. Gharama kubwa za kununua na kuendesha mitambo ya hali ya hewa ambapo sehemu kubwa ya huduma hutolewa bila malipo.

2.2.7 Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ilianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya Mwaka 2001 ili kudhibiti usafiri katika sekta za reli, barabara, bandari na usafiri wa majini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa barabara, pamoja na jitihada mbalimbali za udhibiti zinazofanywa na SUMATRA, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa changamoto mbali mbali zifuatazo;-

a. Kuendelea kuwepo kwa baadhi ya vyombo vya usafiri vibovu na ambavyo si salama kwa kusafirisha abiria;
b. Baadhi ya vyombo vya usafiri kama NOAH ambavyo vimepewa leseni ya kusafirisha abiria chini ya Kilomita hamsini (km 50). Jambo hili limekuwa likilalamikiwa na wananchi kwani vyombo hivi vilikuwa na msaada mkubwa hasa maeneo ambayo ya uhaba wa usafiri;

c. Baadhi ya wamiliki wa mabasi kutoza nauli tofauti na zilizopangwa na SUMATRA; na
d. Mwendo kasi wa baadhi ya vyombo vya usafiri hasa wakati wa jioni au usiku na kuhatarisha maisha ya abiria.

Mheshimiwa Spika, kulingana na tafiti zilizofanyika, asilimia 85 za ajali zinazotokea zinasababishwa na makosa ya kibinadamu kama vile kutokuzingatia alama za barabarani, kutokuwa na elimu ya kutosha katika fani ya udereva, umakini wakati kupita gari jingine (*Overtake*) , ulevi, uchovu na matumizi ya simu za mkononi. Kamati inaona bado kuna haja ya vyombo vinavyohusika kama Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Katiba na Sheria, Wakala wa Barabara Tanzania, Chama cha Wamiliki wa Mabasi, Chama cha Madereva kukaa pamoja na kuona namna nzuri itakayoweza kupunguza changamoto hizi na kuweka mazingira salama kwa wasafiri.

2.3 Sekta ya Ujenzi

2.3.1 Wakala wa Barabara Tanzania- TANROAD

Mheshimiwa Spika, Wakala wa barabara ulianzishwa kwa taarifa ya Serikali iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali Na. 293 mwaka 2000 chini ya kifungu 3(1) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997. Jukumu kubwa la wakala huu ni kuhudumia mtandao wa barabara ambao unakadiriwa kuwa na urefu wa jumla ya kilometa 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometa 22,214 ni barabara za Mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara zetu ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mpango na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa katika kipindi cha Julai- Disemba 2016, jumla ya Kilometa 392.48 za barabara kuu zimejengwa na kilometa 39 zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami pamoja na kukamilisha ujenzi wa madaraja matatu (3). Aidha, Kamati imejulishwa kuwa kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya kilometa 19 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 122.22 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba 2016, utekelezaji wa matengenezo ya barabara kuu na zile za mikoa pamoja na madaraja ulifikia asilimia 30 ambapo kazi zilizofanyika zilijumuisha kilometa 6,852 za matengenezo ya kawaida (*routine and recurrent maintenance*), kilometa 1,151 za matengenezo ya muda (*periodic maintenance*), kilometa 274 za matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*). Vile vile madaraja 870 yalifanyiwa matengenezo ya kawaida na madaraja 71 yalifanyiwa matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Wakala wa Barabara unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

a. Kutokutolewa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo hali inayosababisha kazi zilizopangwa kwa baadhi ya miradi kutotekelezwa ama kutekelezwa kwa kiasi kidogo;
b. Msongamano wa magari barabarani hasa jiji la Dar es Salaam,na miji mingine inayokuwa kwa kasi kama Mbeya, Mwanza na Arusha;
c. Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara;
d. Uwezo mdogo wa Makandarasi wa ndani katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kutokana na kukosa mitaji ya kutosha pamoja na mitambo ya kisasa; na
e. Ongezeko la gharama za ujenzi ambazo ni kikwazo kwa ujenzi wa nyumba za kutosha za gharama nafuu kwa ajili ya makazi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro na mvutano kutoka kwa wananchi mbalimbali unaotokana na wasiwasi wa kutolipwa fidia au kulipwa fidia kwa kiasi kidogo ambacho hakiendani na hali ya uchumi wa sasa jambo linalopelekea wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi.

Aidha, kumeendelea kuwepo uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara ambapo wananchi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya barabara Namba 13 ya Mwaka 2007, hii inaleta usumbufu na gharama kubwa katika ujenzi wa barabara. Ni rai ya Kamati kwamba, vyombo vya usimamizi wa Sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema kuliko kuacha na kusababisha msuguano baadae.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matuta barabarani, licha ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kuahidi kuendelea kurekebisha matuta makubwa ili kuyaweka katika kiwango vilivyoainishwa katika mwongozo wa Wizara kuhusu usanifu wa barabara wa mwaka 2011 *(Road Geometric Design MANUAL, 2011)* bado kumeendelea kuwepo matuta makubwa hasa katika barabara kuu ambapo yamekuwa chanzo cha uharibifu wa barabara kwani magari yenye mizigo hulazimika kwenda mwendo mdogo hivyo uzito kuwa mkubwa na kusababisha barabara kutitia. Aidha, matuta barabarani yamekuwa yakisababisha mizigo kuhama na kuelemea upande mmoja jambo ambalo wakati mwingine limekuwa chanzo cha ajali kwa magari mengi ya mizigo.

a) Barabara za Jiji la Dar es Salaam

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari unaotokana na sababu mbalimbali zikiwemo ofisi nyingi za umma kujengwa sehemu moja na kupelekea wakazi wa jiji kuwa na uelekeo mmoja, ubovu wa barabara za mlisho (*feeder roads*), utegemezi usafiri wa barabara kwa kiasi kikubwa,

uduni wa huduma za usafiri wa umma na ongezeko kubwa la idadi ya magari ikilinganishwa na uwezo wa barabara. Msongamano huu wa magari unaathari nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali zinazofanywa katika kuhakikisha jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Juhudi mbalimbali zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo kasi (BRT), kujenga barabara za juu (*flyovers*) katika eneo la TAZARA na maaandalizi ya ujenzi wa barabara za juu *(Interchange*) katika eneo la Ubungo. Vilevile maandalizi ya ujenzi na upanuzi wa daraja la Selander ambalo litaanzia eneo la Coco Beach hadi eneo la Aga Khan pamoja na kukamilisha barabara zingine za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam.

b) Mizani za Barabarani

Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu ya TANROADS ni ujenzi na utunzaji wa barabara, kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, pamoja na jukumu hilo bado changamoto imekuwa ni uharibifu wa barabara unaosababishwa na magari kubeba mizigo yenye uzito mkubwa. Mfano, magari mengi ya aina ya fuso kwa wastani yanatakiwa kubeba mzigo usiozidi tani 3.5 lakini mengi yanazidisha na kubeba mizigo hadi tani 8. Hali hii ni hatari sana kwani mara nyingi yamekuwa yakisababisha ajali pamoja na uharibifu wa barabara kwani matairi yake ni membamba na huchimba barabara na kusababisha mabonde.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya magari yanayobeba mizigo kupita kiasi yanachostaili, mizani ndicho chombo muhimu sana katika udhibiti uzito wa magari ambayo hupelekea uharibifu wa barabara. Kwa sasa nchini kazi ya udhibiti wa uzito wa magari zinaendelea kwa kutumia mizani 38 ya kudumu, mizani 22 inayohamishika, na mizani mitatu (3) inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion Weghbridge-WIM*).

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa vituo vingi vya mizani bado barabara zimekuwa zikiharibika. Suala hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, Taifa hili litakuwa linaendelea kutenga fedha nyingi kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara zile zile kila mwaka.

Aidha, ili kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, ni vyema sasa katika maeneo ambayo mizani zinakuwa na msongamano mkubwa wa magari kufungwe mizani ya kisasa unaopima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weigh in Motion Weghbridge-WIM*) kama ule uliopo Vigwaza mkoani Pwani ambapo kuwepo kwa mzani huu kumesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza msongamano mkubwa wa magari uliokuwapo katika mzani wa Kibaha kwani na kupunguza malalamiko hasa ya wafanyabiashara.

2.4 Sekta ya Mawasiliano

2.4.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Mheshimiwa spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA ilianzishwa chini ya Sheria Na. 12 ya Mwaka 2003 ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania na Tume ya Mawasiliano Tanzania-*TCC*. Dhumuni la kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini ikiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuendelea kutekeleza ushauri unaotolewa na Kamati katika kipindi cha Januari 2016/ 2017 na hatimae kuweza kufanikisha yafuatayo:-

a. Kuhakiki mawasiliano ya simu za ndani ambapo takwimu za mawasiliano ya ndani yaliyofanyika baina ya watoa huduma za ndani (mwingiliano wa mawasiliano kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine (off-net) kwa mujibu wa Kanuni za Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta za mwaka 2011. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekamilisha mfumo wa *on-net*

traffic monitoring mnamo mwezi Septemba, 2016 ambapo vifaa vilifungwa kwenye makampuni nane (8) ambayo ni Vodacom, TIGO, Airtel.ZANTEL, HALOTEL,TTCL SMART na SMILE na kuunganishwa na mfumo wa usimamizi uliofungwa katika ofisi za TCRA. Aidha, kumbukumbu za mawasiliano ya simu za ndani ya mtandao mmoja (on-net) zilichukuliwa;

b. Kuhamishwa kwa sehemu ya Miundombinu au uendeshaji wa Mitandao ya mawasiliano nje ya nchi ambapo mara baada ya kulibaini hili makampuni matatu ya simu yaligundulika kukiuka Sheria ya Kieletroniki na Posta ya Mwaka 2011.Makampuni hayo yalitakiwa kulipa faini ya **shilingi milioni mia moja (100,000,000.00)** kila moja na kufanya jumla ya faini iliyolipwa kuwa **shilingi milioni mia tatu (300,000,000.00);**

c. Mfumo wa kubaini simu za ulaghai (Antifraud Management System), ambapo simu hizo zimeendelea kutambuliwa na kufungiwa kwani zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa ulaghai na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali; na

d. Kufanya utafiti ili kubaini ukiukwaji wa masharti ya usajili laini za simu za mkononi ambapo makampuni sita yalikuwa yamekiuka masharti hayo hivyo kupewa adhabu ya faini kulingana na makosa yao ambapo jumla ya shilingi milioni miatano tisini na moja (**591,000,000.00**) zililipwa.

2.4.2 Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta

Mheshimiwa spika, mradi wa anuani za makazi unalenga kuanzisha mfumo mpya wa anuani nchini utakaowezesha kuwapo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni kwa kutumia anuani za makazi ujulikanao kama postikodi. Mradi huu ni muhimu sana kwani utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchimi na kisiasa. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mfumo huu uko tayari nchi nzima kinachosubiliwa ni serikali za miji na mitaa kutekeleza katika maeneo husika. Mamlaka imeweka postikodi maeneo ya mfano katika jiji la Arusha, Dodoma na Dar Salaam ambapo imeweka namba za nyumba na majina ya mitaa. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa kutokuwa na mipango miji na ujenzi holela, na pia upatikanaji wa majina ya mitaa, kutokana na mabishano juu ya majina katika ngazi ya Halmashauri husika.

Vilevile, changamoto nyingine zinazoukabili mradi huu ni kutokuwa na fedha za kutosha, kutokuwepo kwa takwimu halisi za idadi ya barabara/mitaa katika kata, kutokuwepo kwa takwimu na taarifa halisi za makazi na wakazi katika Kata na uharibifu wa miundombinu kama vile nguzo za majina ya mitaa na vibao vya namba za nyumba hata sehemu zilizopangwa.

Mheshimiwa spika, kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Kamati ilipopata taarifa hii mwezi Machi, 2016 fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hazikuwa zimetolewa. Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga **shilingi bilioni 3 (3,000,000,000.00**) kwa ajili ya uendelezaji wa mradi katika mji wa Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza na Mbeya.

2.4.3 Shirika la Posta Tanzania

Mheshimiwa spika, shirika hili linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani uliopo na changamoto ya soko katika sekta ya posta. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeendelea kufanyia kazi Shirika hili ili liweze kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa madeni mbalimbali. Aidha, shirika lililipa kiasi cha **shilingi billion 5** kwa ajili ya kulipa *pension* za wastaafu wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki kwa niaba ya Serikali kwa makubaliano ya kurejeshewa fedha husika na Serikali.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na hatimae kuanza kulipa deni hili ambapo mpaka sasa Serikali imelipa kiasi cha **shilingi bilioni 1.7.**

Mheshimiwa spika, kufuatia hali mbaya ya kifedha Shirika limeshindwa kulipa madeni ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA ilikamata akaunti za shirika mara tatu kati ya Desemba 2015 na Februari 2016 kwa wakati tofauti kwa limbikizo la **takribani bilioni 15**. Aidha, Shirika kuwekwa kwenye orodha ya mashirika yanayokusudiwa kurekebishwa kumesababisha Shirika kushindwa kupata kibali cha kukopa fedha kwa taasisi za fedha kwa ajili yakuongeza mtaji na kuendeleza rasilimali za Shirika na kutoa huduma zake.

2.4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

Mheshimiwa spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote Kamati imejulishwa kuwa mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara. Changamoto kubwa ni watoa huduma wengi wa simu kutokushiriki kikamilifu katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa, kumekuwepo na mafanikio mbalimbali kupitia utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini ambapo katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2016/2017, Mfuko wa Mawasiliano ulifikisha huduma za mawasiliano katika kata 138 zenye jumla ya vijiji 557 na kata 443 zinafikishiwa huduma ya mawasiliano kwa kutumia ruzuku ya Serikali ambapo kata 122 bado hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia sekta ya Mawasiliano iliingia mkataba na Kampuni ya simu ya Viettel ili kufikisha mawasiliano vijijini ambapo Kampuni hiyo ilitakiwa kufikisha mawasiliano kwenye vijiji 4,000 ndanii ya miaka mitatu. Hadi kufika Desemba 2016 Kampuni ya Viattel ilifikisha mawasiliano katika vijiji 2,889 kati ya vijiji 3,000 vilivyotakiwa kufikiwa. Kuchelewa kukamilisha kumechangiwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa vibali vya ujenzi katika maeneo

ya minara. Awamu ya tatu ya mradi huu inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2017. Kampuni ya Viettel imebakiza vijiji 1,178 ambavyo vinapaswa kukamilika hadi kufikia mwezi Novemba 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na muda ambao mfuko huu umekuwepo toka kuanzishwa kwake, Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Kamati imebaini kuwa Makampuni makubwa ya simu bado hayajaimizwa vya kutosha kupanua huduma zao katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara kama mojawapo ya uwajibikaji wao kwa jamii (*corporate social responsibility*). Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku kuyafikia maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara ili kuyafikia yote kwa haraka zaidi utaratibu wa kuzitaka Kampuni kubwa kuonekana zinasaidia ni jambo sahihi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI

3.1 Bajeti ya Miundombinu

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuendeleza miundombinu nchini ambapo kwa mara ya kwanza Sekta ya Miundombinu katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 imetengewa **asilimia 16.7** ya bajeti yote ya Serikali. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kutoa fedha kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni

3.2 Sekta ya Uchukuzi

3.2.1 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Bandari Tanzania, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ni kiungo muhimu kati ya nchi yetu na nchi jirani ambazo hazina bahari (*land lock countries*); na kwa kuwa bandari hii ikiimarishwa itaweza itaweza kuingizia nchi yetu mapato mengi zaidi na hata kukuza uchumi; Kamati inashauri Serikali kuboresha mazingira ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza kina katika gati namba 1-7, upanuzi wa lango la kuingilia meli, kujenga gati namba 13 & 14 pamoja na kuimarisha usafiri wa njia ya reli kutoka bandarini. Vilevile Mamlaka ya Bandari Tanzania iwe na mkakati wa kutangaza maboresho hayo na huduma zake kuliko ilivyo sasa.

b) Aidha, Kamati inashauri changamoto zifuatazo zifanyiwe kazi kwa kina ili kuongeza ufanisi wa Bandari nchini:-

i. Hofu ya wateja kutokana na kuanzishwa kwa Sheria ya (*Value Added Tax-VAT)* kwa huduma zitolewazo na mawakala kwenye mizigo ya nchi jirani *(VAT on transit goods*) ambayo ni kinyume na Sheria za Kimataifa.

Uwepo wa Sheria hii unawafanya wateja kutotumia bandari za Tanzania kwa sababu ya gharama;

ii. Mgongano wa tozo za hifadhi za mizigo *'Customs Warehouse Rent"* inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA na *'Storage Charges"* zinazotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA. Malipo haya yanafanana isipokuwa yametofautiana majina tu, hivyo wafanyabiashara kuona kuwa wanalipa mara mbili igharama ya hifadhi za mizigo;

iii. Tozo za barabara (*Road Tolls*) ambapo hutozwa **Dola za Kimarekani 16** kwa Kilomita ukilinganisha na **Dola za Kimarekani 8** kwa Kilomita zinazotozwa katika nchi zenye bandari shindani;

iv. Tozo ya **Dola za Kimarekani 23** kwa tani kwa mzigo wa shaba ambapo bandari nyingine shindani kama Durban hutoza Dola za **Kimarekani 17.86**;

v. Kwa mujibu wa makubaliano ya mwanzo, tozo kubwa kwa mizigo yote inayotoka ama kwenda Zambia tofauti na tozo za nchi nyingine kama Rwanda na Burundi. Mfano, kasha la *urefu wa futi 40* linatozwa **Dola za Kimarekani *530*** kwa mzigo wa Zambia badala ya **Dola za Kimarekani *320*** ambazo hutozwa kwa kasha hilo hilo linalokwenda Rwanda ama Burundi;

vi. Himaya ya forodha kwa pamoja (*Single Customs Territory*) kwa mzigo wa Congo umeleta utata na kupunguza motisha kwa wafanyabishara wa nchi hiyo kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Hii inatokana na kuwa mfumo wa ukusanyaji kodi ndani ya DRC unatoa mwanya kwa baadhi ya wafanyabiashara katika nchi hiyo kutolipa kodi kwa asilimia mia moja (100%) tofauti na mizigo inayopatikana kwenye mfumo wa *''Single Customs Territory"* ambayo hutozwa kodi kwa asilimia mia moja (100%) jambo linalosababisha baadhi ya wafanyabiashara wa Congo kuona gharama kubwa kupitisha mizigo yao Tanzania;

vii. Muda mfupi (*Short grace period of Transit Bulk liquid*) kwa mzigo wa mafuta wa nchi za jirani (Siku 30) bila kujali mazingira ya usafirisha wa barabara katika nchi yetu tofauti na nchi nyingine shindani ambazo ni siku 60 hadi 90 na utaratibu duni;

viii. Mfumo wa TANCIS wa TRA kutokurushu kugawanya "*Bill of Lading*" ili kuruhusu kutoa mizigo ambayo haina tatizo panapokuwa na tatizo la Mzigo Moja badala ya mzigo wote kuzuiwa na kusababisha gharama za tozo za hifadhi kwa mteja ambazo sio za lazima;

ix. Kuongezeka kwa Tozo kutokana na "*Government Chemical Agencies*" kutoza USD 1.00 Kwa Tani badala ya USD100 Kwa "Bill of lading" kwa bidhaa ambazo wanazikagua kama vile mbolea na hivyo kuongeza kutoka wastani wa USD 500 hadi USD 20,000 au zaidi kutokana na ukubwa wa mzigo;

x. Idara za Serikali (OGD's) na Mabenki kutokufanya kazi masaa 24 /7. Utendaji wa bandari unategemea upatikanaji wa vibali kutoka idara za mbalimbali za serikali pamoja na huduma za kibenki;

xi. Usalama mdogo wa mizigo inayosafirishwa kwenda nchi za jirani (wizi wa mizigo na madereva kuvamiwa) na hivyo wenye mzigo kulazimika kuingia gharama ya kuweka walinzi wa kusindikiza mizigo; na

xii. Gharama kubwa za usafirishaji kwa njia ya barabara inayochangiwa na wingi wa vituo vya ukaguzi "*check Points*" na malipo yanayodaiwa na watendaji wasio waaminifu.

c) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari kavu- ICD's, Kamati inapongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa kujenga bandari kavu itakayomilikiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) katika eneo la Kwala-Wilayani Kisarawe kwani kwa kiasi ICD's zinazomilikiwa na watu binafsi uchelewashaji na upotevu wa mizigo pamoja na ukwepaji wa kodi.

d) **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwapo kwa udanganyifu unaofanywa na mawakala (*freight forward*) kwa kuongeza gharama kwenye hati za madai zinazotumwa kwa wateja. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa mawakala wanaobainika kuongeza gharama hizo ikiwezekana wafutiwe leseni zao;

e) Kwa kuwa miongoni mwa kero za wafanyabiashara wanautumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwepo kwa maegesho ya magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini; Kamati inashauri Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kushirikiana na Halamshauri ya Wilaya ya Temeke kushirikiana na kuhakikisha eneo lililokuwa limetengwa kwa ajili ya maegesho linapatikana.;

f) **Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya unaendelea; Kamati inasisitiza kuwa suala hili lipewe kipaumbele ili mchakato huo uweze kukamilika haraka kwani ni muhimu kufahamu kiasi cha mafuta kinachoingia na kutoka ili kuweza kutoza kodi stahiki;

3.2.2 Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge;*

Kwa kuwa sasa Serikali imeonesha nia ya kutaka kuifufua reli ya kati na kuijenga katika kiwango cha kisasa kwa kutenga katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2016/2017 **shilingi trilioni 1;** na kwa kuwa wakati nchi yetu inajiandaa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge,* nchi zingine wanachama wa Afrika Mashariki zinaendelea kujenga kwa kasi kubwa sana reli kwa kiwango cha *Standard gauge* kutoka Mombasa-Nairobi- Kampala hadi Kigali.;Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

a) Serikali kuharakisha ujenzi wa reli ya kati na matawi yake ambayo ni kutoka Dar es Salaam – Kigoma, Uvinza - Msongati kwa ajili ya mzigo wa Burundi; tawi la Tabora- Kalemi kwa ajili ya mizigo ya DRC; na Tabora- Shinyanga- Mwanza kwa ajili ya ukanda wa ziwa. Aidha, Kamati inashauri Serikali pia kuanza kufanya utafiti wa kupanua matawi *(spurs*) ya reli ya kati kutoka Bandari kavu ya Isaka (Shinyanga) hadi Rusumo Mkoani Kagera, hivyo kuwezesha mradi wa kuchimba madini ya *Nickel* huko Kabanga kutekelezeka.

b) Ni vyema mradi huu wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge,* Serikali uipe Kampuni moja ili yenyewe ijigawe kadri inavyoweza badala ya kujenga vipande vidogo vidogo na Kampuni tofauti. Ikiwa reli hii itajengwa na Kampuni moja itasaidia katika viwango vya reli itakayojengwa. Vilevile, Serikali itangaze rasmi muda wa kuanza na kukamilisha kazi ya ujenzi wa reli hii na matawi yake.

c) Uimarishwaji wa reli uende sambamba na kutafuta suluhisho madhubuti katika maeneo korofi kama vile stesheni ya Kilosa- Gulwe Morogoro kwani tatizo la kuharibika eneo hili kwa reli kusombwa na maji limekuwa linajirudia mara kwa mara na kugharimu fedha nyingi bila kupata suluhisho la kudumu.

d) Serikali iimarishe karakana za treni nchini ili kutoa wataalam watakaoweza kuhudumia reli zetu kwa ufanisi na kwa namna endelevu.

3.2.3 Mheshimiwa Spika, kuhusu kuunganisha Mashirika ya Serikali RAHCO na TRL, TPA na MSCL;

Kwa kuwa lengo zuri la Serikali kutenganisha mashirika yake ya RAHCO na TRL pamoja na TPA na MSCL limeshindwa kufanikiwa kwa sababu ushindani uliotegemewa haukupatikana (*Market Failure*). Kamati inashauri Mashirika haya yaunganishwe ili Mashirika yake mama yasaidiane na mashirika ya

huduma ambayo mpaka sasa yanatengeneza hasara (*cross-subsidization*) na yanahitaji kusaidiwa na shirika mama.

3.2.4 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia-TAZARA

Kwa kuwa utendaji wa TAZARA umekuwa ukishuka siku hadi siku; na kwa kuwa moja ya sababu ya TAZARA kushuka ni mapungufu yaliyopo katika Sheria Na.4 ya Mwaka 1975; Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

a) Serikali ihakikishe inakamilisha utaratibu mpya waliokubalina kati yake na Zambia juu ya uendehaji wa Shirika la TAZARA. Vilevile, Serikali iendelee kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha kwenye Shirika hili; Aidha, Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi pamoja na kuhakikisha makato ya wafanyakazi yanayopelekwa katika mifuko ya hifadhi jamii ili kuepuka usumbufu kwa wafanyakazi wanaostaafu;

b) TAZARA kubuni mbinu za kujiendesha kibiashara ikiwemo kuangalia upya bei zake kwani wafanyabiashara wengi wamehamia kwenye usafiri wa barabara kwa kuwa ni nafuu zaidi ukilinganishwa na usafiri wa treni. Mfano, gharama za kusafirisha mbao kutoka mbeya kwa gari ni shilingi 2,000,000 mzigo unafika mpaka sehemu ya biashara ukilinganishwa na behewa moja linalokodiwa kwa kiasi cha shilling 3,600,000 na bado kuna gharama za kupeleka mzigo kupakia na baadae kushusha kupeleka sehemu ya biashara;

c) Serikali kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya vichwa sita (6) ambavyo vinasubiri matengenezo kwa gharama ya inayokadiriwa kuwa shilingi billion 6;

d) Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafishaji wa makaa ya

mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kupatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha;

e) Serikali kuimarisha manajimenti ya kiwanda cha kokoto cha kongoro ili kiweze kujitegemea kwani sahivi zaidi ya asilimia 60 ya kokoto zinazozalishwa hapo hutumiwa na TAZARA na kiasi kidogo kinauzwa kwa watu binafsi na hata ikiwezekana kijitegemee ili Tazara wawe wanakwenda kununua kununua kokoto hizo kwani wameshindwa kuweka mtaji kwa ajili ya kukiendeleza.

3.2.5 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA

Kwa kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inatoa mchango mkubwa katika mapato yatokanayo na viwanja vya ndege nchini, na kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa ya uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege, Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Serikali kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege angalau **asilimia 50** ya maduhuli (*retention)* yatokanayo na viwanja vya ndege ili kusaidia kuongeza kasi ya shughuli za Mamlaka zikiwemo ukarabati na upanuzi wa viwanja vikiwemo Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Kiwanja cha Ndege cha Arusha, Kiwanja cha Ndege cha Moshi, Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Kiwanja cha Ndege Musoma, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga Kiwanja cha Ndege cha Mpanda na Kiwanja cha Ndege cha Nduli- ringa. Vile vile, kuweza kulipa fidia kwa viwanja vya ndege vya Julius Nyerere International Airport- JNIA, Mwanza, Bukoba, Omukajunguti, Msalato, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Sumbawanga, n.k

b) Serikali ihakikishe inamaliza kwa wakati malipo ya fedha yaliyoidhinishwa kwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara;

c) Kamati inashauri Serikali kuharakisha kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu *(Termina III*) la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili mradi huu uweze kukamilika katika muda uliopangwa yaani Disemba 2017. Aidha, Kamati inashauri wakati ujenzi wa jengo la tatu unaendelea, ni vyema kuendelea kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria linalotumika sasa ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi;

d) Pamoja na kwamba Serikali imeanza kutekeleza ushauri wa Kamati wa kubadilisha umiliki wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro kutoka KADCO kwenda TAA ambapo hatua iliyofikiwa ni kuweka kumbukumbu sahihi za taarifa na mizania zilizopo BRELA na taratibu za kisheria za kuondoa mikataba miwili iliyobaki (*Concession Agreement na Lease Agreement*). Kamati inasisitiza kuharakishwa kwa mchakato huu ili Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kirejeshwe kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA na kiweze kuongeza ufanisi, tija na mapato;

e) Pamoja na kwamba Serikali kwa kiasi imezingatia utekelezaji wa maaagizo ya Kamati kuhusu kupima viwanja vyake, ambapo hadi sasa Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege vinane (8) vimeshapatiwa hati miliki, bado kuna haja ya kuhakikisha kuwa viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na kuwekwa uzio ili ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro na wananchi na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kwa ajili ya fidia; na

f) Kuhusu viwanja vya ndege kujengwa na TANROADS, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia Sheria na Mamlaka ya uanzishwaji wa vyombo hivyo viwili. Kwamba kwa mujibu wa uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA ndiyo Taasisi ya Serikali ya kusimamia na kuendeleza Viwanja vya Ndege. TANROADS majukumu yake ni kusimamia barabara zilizo chini yake kwa mujimu wa sheria. Hivyo, Serikali iimarishe uwezo wa Mamlaka ya

Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA na si kuyahamisha majukumu ya Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania kwa Mamlaka nyingine. Kamati inaona wazi kuwa ueledi wa barabara uko TANROADS na ueledi wa ujenzi wa viwanja vya ndege uko kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege-TAA.

3.2.6 Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL

Kwa kuwa Serikali imechukuwa hatua ya kufufua Shirika la ndege la Tanzania kwa kununua ndege mbili mpya aina ya Dash 8-Q400 na kwa kuwa kuna mpango wa kuongeza ndege nyingine mpya mbili (2) zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya watu 155; na kwa kuwa ndege hizo kwa vyovyote vile zitakuwa kichocheo cha Uchumi wa Tanzania katika kuwawezesha watanzania kupata usafiri wa haraka na hivyo kutimiza malengo katika nyanja mbalimbali za uchumi.Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Mafunzo ya menejimenti ya biashara ya ndege (kwa kwenda nchi zilizofanikiwa hasa China), hasa kwa viongozi wa bodi na viongozi wakuu wa Kampuni ya Ndege-ATCL ili waje na mawazo ya kisasa yatakayowawezesha kuingia katika ushindani wa kibiashara. Ikumbukwe kuwa mikakati ya ATCL pia inafanywa na washindani wake;
b) Mifumo ya uendeshaji wa shirika iwe yenye malengo chanya yenye kupelekea kuleta mabadiliko katika sekta ya usafiri wa anga;
c) ATCL sasa ijitangaze kwenye vyombo rasmi vya kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima ya GDS kama Galileo na Amidius ili kutoa huduma bora za usafiri wa anga ndani na hata kimataifa, Kamati inashauri ; na
d) Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ijipange kuingia katika soko la usafiri wa anga na kuhakikisha abiria wengi zaidi wanatumia usafiri wa ndege zake hii ikiwa pamoja na kuendelea kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali, kujali wateja *(costomer care)* na kuwa gharama nafuu za nauli.

3.2.7 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania –TCAA

Kwa kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ni Mamlaka yenye jukumu la udhibiti katika sekta ya usafiri wa anga nchini (kama inavyosimamiwa na sheria ya usafiri wa Anga CAP 80 (R.E 2006)), na kwa kuwa kumekuwa kukitokea changamoto mbalimbali katika usafiri wa anga hasa pale ndege zinapohairisha ama kufuta safari ghafla, Kamati inashauri kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga ifanye kazi zake vyema kwa kuhakikisha kuwa inatoa elimu kwa umma na inakuwa na dawati la kufuatilia malalamiko kutoka kwa abiria pamoja na kutangaza namba za simu na hata kuzionesha kwenye tiketi za ndege za abiria;

Vilevile, Kamati inashauri Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) itengeneza Kanuni zenye kuakisi Sheria na Kanuni za Kimataifa za usafiri wa anga ili kuwatendea haki abiria hasa pale ndege zinapohairisha au kufutwa safari;

3.2.8 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania-TMA

Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali itenge fedha ili Mamlaka hii iweze kuimarisha miundombinu yake ya utendaji kazi kama kujenga jengo lake, kuwa na vifaa vya kutosha sambamba na ukarabati na kuongeza idadi ya vituo vya kupimia hali ya;

b) Serikali kutoa ruzuku kwa ajili ya kusomesha wataalam wa hali ya hewa *(meteorologist)* ili kuweza kukabiliana na uhaba wa wataalam wa hali ya hewa wenye wenye shahada ya kwanza ambayo ndicho kigezo ama matakwa ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

3.2.9 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*Surface and Marine Transport Regulatory Authority-(SUMATRA)*

Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kwa kuwa kumekuwepo tatizo la upandishaji nauli kiholela na kwa kuwa tatizo hili limekuwa likiathiri wananchi hasa wa pembezoni, Kamati inashauri SUMATRA ihakikishe kuwa inafatilia nauli za maeneo mbali mbali nchini ili wananchi wapate auheni ya usafiri hususani maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi kama Mpanda, Tabora, Kigoma na Mtwara;

b) Kwa kuwa SUMATRA kisheria ndio wamepewa jukumu la kuhakikisha magari yanayobeba abiria yanakidhi ubora wa kusafirisha abiria, na kwa kuwa teknolojia imekuwa ikibadilika mara kwa mara, Kamati inashauri Serikali kupitia SUMATRA ianze kuona uwezekano wa kuwa na vituo vya kisasa vya ukaguzi wa magari kwa kila kanda kwani itasaidia kuongeza Pato la Serikali na kuondoa usumbufu kwa wananchi; na

c) Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la ajali za pikipiki, na kwa kuwa ajali hizi zimekuwa zikiathiri sana wananchi kwani wengi wamekuwa wakipoteza viungo vya mwili na hata kubaki kuwa watu wenye ulemavu, Kamati inashauri SUMATRA itoe mafunzo ikiwezekana nchi nzima ukianzia maeneo yale ambayo ajali za pikipiki ni nyingi ili kusaidia kupunguza madhara yatokanayo na ajali hasa za pikipiki; na

d) Kamati inashauri SUMATRA iangalie uwezekano wa kuruhusu aina ya vyombo vingine vya usafiri kama Noah katika utoaji wa huduma ya usafiri hasa katika maeneo yaliyoko vijijini.

3.2.10 Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Usafirishaji Tanzania –NIT

Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kwa kuwa Chuo cha Usafairishaji Tanzania ni Chuo cha Serikali na kwa kuwa kinatoa elimu ya kipekee hapa nchini, Kamati inashauri Serikali kupeleka nguvu Chuo cha Usafirishaji Tanzania (NIT) ili kuboresha miundombinu ya Chuo hasa majengo na magari ya kufundishia. Vile vile, Serikali iharakishe kulifanyia kazi andiko lenye lengo la msaada wa kupanua Chuo toka Serikali ya China; na

b) Kwa kuwa Chuo cha Usafirishaji – NIT kinatoa mafunzo muhimu na ya kipekee kama mafunzo ya uhandisi wa ndege, na kwa kuwa gharama ya ada kwa ajili ya mafunzo haya ni kubwa, Kamati inashauri Serikali itoe ruzuku kwa kozi ambazo ni za kipekee na ambazo ada zake ni ghali ili kuweza kupata wanafunzi wengi na hatimae kuwa wataalam wengi; Aidha, Serikali sasa iboreshe Miundombinu ya Vyuo hivi ili viweze kuvutia watu wengi toka ndani na nje ya nchi kujiunga na kupata elimu katika vyuo hivi;

3.2.11 Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI)

Kwa kuwa Vyuo vinavyofundisha elimu ya bahari Afrika vipo vinne tu pamoja na Chuo cha Bahari Dar es Salaam, na kwa kuwa mafunzo haya yanaongeza tija na ufanisi; hivyo basi Kamati inaishauri Serikali iongeze ruzuku kwenye Chuo cha Bahari Dar es Salaam ili kukarabati karakana ya kufundishia ili iweze kufanya kazi na Chuo kiweze kujitegemea na kutoa mafunzo kwa wanafunzi wengi na kuwapa ajira watanzania wengi.

3.3 Sekta ya Ujenzi

3.3.1 Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Barabara Tanzania-TANROAD

a) Kwa kuwa malengo ya Sekta ya Ujenzi ni pamoja na kujenga barabara kuu ili kufungua fursa za maendeleo na kuhakikisha miji yote mikuu na mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo 2017/18; na kwa kuwa lengo hili bado halijakamilika kutokana na Mikoa mingine ambayo haijaweza kuunganishwa kwa barabara ya lami; Kamati inashauri Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Njombe-Makete-Mbeya nayo iunganishwe ili kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo hayo. Vilevile, Serikali ikarabati baadhi ya barabara za Mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;

b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama runinga, magazeti na redio. Pia kufanya mikutano na kuweka alama zitakazoonesha mwisho wa eneo la barabara;

c) Serikali kuendelea na ujenzi wa barabara hasa kwa barabara zile zinazounganisha nchi yetu na nchi za jirani, mikoa, wilaya na maeneo ya uzalishaji kama vile kilimo, madini na viwanda;

d) Serikali iendelee kuzingatia kuoanisha uendelezaji wa miundombinu na mipango miji;

e) Matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa zinasababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalumu;

f) Ili kuilinda miundombinu yetu hasa alama za barabara na reli; upo umuhimu mkubwa wa kutungwa kwa Sheria ya kudhibiti uuzaji wa chuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu; na

g) Serikali inunue mizani ya kisasa ambazo zinauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weight in Motion*). Kamati inaendelea kushauri mizani hizi za kisasa zifungwe pia katika maeneo mengine yanye kusababisha msongamano mkubwa wa kupima magari Mfano, Himo-Moshi, Mizani ya Mikese- Morogoro, Kihonda-Morogoro, makambako, kwa mpemba n.k. Kamati inashauri adhabu kali zitolewe kwa wanaozidisha uzito wa mizigo ili iwe fundisho kwa wengine.

3.3.2 Mheshimiwa Spika, kuhusu kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam;

a) Kwa kuwa Serikali imeonesha nia ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam kwa kuweka barabara za juu (*flyovers*) eneo la TAZARA na Ubungo, na kwa kuwa msongamano katika jiji la Dar es Salaam hautaweza kupunguzwa kwa barabara za juu katika maeneo hayo mawili tu; Kamati inashauri barabara za juu maarufu kama (*flyovers)* zijengwe hasa katika makutano ya barabara kuu zenye msongamano mkubwa kama vile, Magomeni, Morocco, Mwenge, Kilwa Road, Makutano ya Kenyata, Kinondoni na Ali Hassan Mwinyi Road na Kamata. Kamati inaona ni vyema ikiwa Serikali itahusisha Sekta binafsi na Mifuko ya Pension katika ujenzi wa barabara hizi za juu (*flyovers*) ili iweze kukamilika kwa haraka. Aidha, kamati inasisitiza umuhimu wa upanuzi wa daraja la Salenda na daraja la gerezani;

b) Ili kupunguza msongamano katika jiji la Dar es salaam, ni muhimu kukamilisha ujenzi wa barabara zinazosaidia wananchi kufika maeneo yao bila kupita katikati ya Jiji la Dar es salaam, ikiwa ni pamoja kukamilisha barabara kutoka Goba-Madale-WazoHill, Goba –Kimara, Ardhi-Makongo-Goba n.k. Pia barabara za mitaani *(ring roads)* nazo zifunguliwe kwa kuwekwa lami kwani zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa; pia

c) Katika juhudi za kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, ni vyema Serikali kuamua sasa kuwa na vituo vitatu katika kila barabara kuu kama vile, kutoka Dar Es Salaam kwenda Rusumo, Dar Es Salaam kwenda Namangana Dar Es Salaam kwenda Tunduma.

3.3.3 Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Majengo Tanzania-TBA;

Kamati inashauri Serikali kuimarisha uwezo wa TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Vilevile Kamati inashauri Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili.

3.3.4 Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha matumizi stahiki ya nguvu kazi Mbeya (*Appropriate Technology Training Institute-ATTI*);

Kamati inashauri Serikali iviunganishe vyuo hivi na kuvisajili ili mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi yaweze kutambulika. Aidha, Serikali ivitengee bajeti ya kutosha vyuo hivi ili viweze kuwa na mvuto kwa watu wengi kujiunga na kupata elimu kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalam hasa wa barabara katika Halamashauri nchini ambapo wataalam hao wanategemewa kutoka katika vyuo hivi;

3.4 Sekta ya Mawasiliano

3.4.1 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA;

Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuharakisha kutafuta ufumbuzi wa namna bora ya kupata taarifa za makusanyo ya simu za ndani kwa kutumia mtambo wa *TTMS* ili Serikali iweze kutoza kodi stahiki kutokana na miamala ya fedha inayofanyika kupitia simu

za mkononi. Kuendelea kuchelewa kulitekeleza suala hili kunazidi kuikosesha nchi kodi stahiki kutokana na Makampuni haya kutotozwa kodi stahiki;

b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na

c) Serikali kupitia TCRA ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA iendelee kuisaidia Jeshi la Polisi katika kutekeleza sheria ya *Cyber Crime* na kuwabana wahalifu.

3.4.2 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF;

Kwa kuwa mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kupeleka mawasiliano sehemu zisizokuwa na mvuto wa kibiashara; na kwa kuwa Kamati bado hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa mawasiliano sehemu hizo; Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Katika Bajeti ijayo ya mwaka 2017/2018, Serikali kuzingatia kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, kwani ruzuku inayotolewa na Serikali ikitumika vizuri inaweza kusaidia zaidi kuliko kupewa Makampuni ambapo mwisho wa siku hawapeleki mawasiliano;

b) Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA kuweka masharti ya kutoa leseni kwa Makampuni ya Simu pamoja na masharti mengine iwe kupeleka mawasiliano katika maeneo ya pembezoni kama mchango wa kijamii (*Corporate Social Responsibility);*

c) Serikali kuja na mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo linalohatarisha usalama.

3.4.3 Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta;

Kwa kuwa mradi huu unamanufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimae kurahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa; na kwa kuwa kwa kuwa utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukisuasua; hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa; na

b) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe mapema kwani hadi kufikia mwezi Januari 2017 zimetolewa **asilimia 3.17** tu ya Fedha iliyoidhinishwa.

3.4.4 Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL;

Kwa kuwa Serikali imekamilishaa malipo ya hisa ya **asilimia 35** zilizokuwa zinamilikiwa na *Bharti Airtel* katika TTCL; na kwa kuwa sasa Kampuni hii inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja (100%); Kamati inashauri TTCL kuhakikisha inaboresha makusanyo ya mapato na madeni yanayotokana na huduma za simu ambayo kwa kiasi kikubwa wateja wanaodaiwa ni Serikali na taasisi zake;

Aidha, Kamati inashauri Kampuni hii ipate dhamana ya mikopo na kuweza kujiimarisha na kuongeza ufanisi

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mh.Spika, Miundombinu ikiwa ni pamoja na Reli, Barabara, Viwanja vya Ndege, Bandari na Mawasiliano ni nguzo ya Taifa lolote na kwa kweli ndiyo vichochezi vya maendeleo ya sekta zingine. Hivyo, ni lazima tutambue kuwa maendeleo ni vita na lazima tupange mipango yetu kama tungapavyo vita yoyote ile. Kosa moja lawezi kugharimu uchumi wan chi yetu. Lazima tuamue kwa usahihi na kwa muda muafaka ili kupata maendeleo.

4.1 Shukrani

Mheshimiwa spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Prof. Makame Mbarawa Mnyaa (Mb) akishirikiana na Naibu Waziri Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani (Mb), pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara hii Eng. Joseph Nyamuhanga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndg.Angelina Madete. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani ziwaendee makatibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuihudumia Kamati muda wote. Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo, sasa naomba kutoa Hoja kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja.

.....

Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mb
Mwenyekiti
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
07 Februari, 2017

KIAMBATISHO NAMBA 1;

SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017

Na	Kipindi cha Utekelezaji	Shughuli zilizofanyika	Dhumuni
1.	08-12, Februari 2016	Mafunzo *(Training)* kwa Wajumbe wa Kamati	Kuwajengea uwezo wajumbe (*Capacity Building*) katika maeneo wanayoyafanyia kazi hasa kuhusu Muundo, Majukumu, Sera na Sheria za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
2.	13 Machi - 24 Aprili 2016	a) **Vikao na Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara**; i. Wakala wa Barabara Tanzania – TANROADS; ii. Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA; iii. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA; na iv. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA. b) **Ziara Taasisi/Mashirika yaliyochini ya Wizara** i. Ziara eneo la Soga-Kibaha lililojengwa (1.5 km za reli ya *standard gauge*); ii. Karakana ya Vichwa vya Treni Morogoro na Ofisi za Railway Dodoma; iii. Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, Shinyanga na Mwanza; iv. Barabara ya Nzega- Tabora, v. Bandari ya Mwanza	Kupokea taaarifa ya utendaji wa baadhi ya Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

3.	29 Machi-05 Aprili 2016	**Ziara za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo:-** i. Mradi wa ujenzi jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam; ii. Mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni; iii. Mradi wa upanuzi wa Barabara ya Kimara-Kibaha (25.7 Km) na mradi wa ukarabati wa barabara ya Mlandizi-Chalinze (42 km); iv. Mradi ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe; na v. Ziara mradi wa ujenzi wa barabara Mbeya-Lwanjilo (36km) na mradi wa ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongorosi	Kwa mujibu wa Kanuni ya {Kanuni ya 98 (1)}. Kutembelea miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka 2015/2016 ili kujiridhisha na utekelezaji uliofikiwa.
	08 -15 Aprili 2016	Kupokea na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2016/2017 i. Sekta ya Mawasiliano Fungu 68; ii. Sekta ya Ujenzi Fungu 98; na iii. Sekta ya Uchukuzi Fungu 62.	Kupokea na kujadili taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
	22 Agosti- 02 Septemba 2016	**Vikao na Mashirika/Taasisi zifuatazo**:- i. Shirika la Ndege la Tanzania-ATCL; ii. *Tanzania Electrical Machenical and Electronics Service Agency*-TEMESA; iii. Kutembelea Kiwanja cha Ndege cha Dodoma; iv. Wakala wa Majengo Tanzania-TBA, Railway Holding Company (RAHCO); v. Tanzania Railway Limited (TRL); vi. Tanzania and Zambia Railway (TAZARA);	Kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo

		vii. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA; viii. Kampuni ya Simu Tanzania- TTCL; na ix. *Kilimanjaro Airport Development Company Limited*- KADCO	

	17-30 Oktoba, 2016	**Vikao na Mashirika/Taasisi zifuatazo**:-
		i. Wakala wa Barabara (TANROADS);
		ii. Chuo cha Ujenzi Morogoro;
		iii. Chuo cha Matumizi Stahiki ya Nguvu Kazi Mbeya (*Appropriate Technology Training Institute-ATTI*);
		iv. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);
		v. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund - UCSAF);*
		vi. Mamlaka ya Bandari Tanzania(TPA);
		vii. *Marine Services Company Limited (MSCL)*;
		viii. Kampuni ya Meli ya Tanzania na China (SINOTASHIP);
		ix. Chuo cha Usafirishaji Tanzania(NIT);
		x. Chuo cha Bahari Dar es salaam (DMI);
		xi. Kampuni ya Ndege Tanzania-ATCL;
		xii. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA);
		xiii. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA); na
		xiv. Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*Surface and Marine Transport Regulatory Authority-(SUMATRA)*
			Kupokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo

	10-14 Januari 2017	Ziara ya kutembelea Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia-Mbeya	Wajumbe kuona, kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa TAZARA
	17- 29 Januari 2017	**Ziara kutembea Mashirika/ Taasis zifuatazo:-** i. Kiwanja cha Ndege cha Arusha , Moshi na Kilimanjaro (KIA); ii. Bandari ya Tanga iii. Eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mwambani-Tanga;	Wajumbe kuona, kupokea na kujadili taarifa ya utendaji wa Mashirika/Taasisi ili kushauri ipasavyo

		iv. Eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mbegani-Bagamoyo; **c) Vikao** i. Mamlaka ya Bandari Tanzania-TPA (Bandari ya Dar es Salaam); ii. Kupokea taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Mawasiliano; iii. Kupokea taarifa ya utendaji wa sekta ya Uchukuzi; iv. RAHCO- *Railway Holding Company*; v. Wakala wa Ndege za Serikali	

KIAMBATISHO NAMBA 2;

JEDWALI LA VIFUPISHO (*ABBREVIATIONS*)

TAZARA	-	Tanzania and Zambia Railway
SUMATRA	-	Surface and Marine Transport Regulators Authority
TPA	-	Tanzania Ports Authority
TMA	-	Tanzania Meteology Agency
TEMESA	-	Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency
TTCL	-	Tanzania Telecommunication Company Limited
TCC	-	Tanzania Communication Commission
UCSAF	-	Universal Communication Services Access Fund
TBA	-	Tanzania Building Agency
MSCL	-	Marine Services Company Limited
DMI	-	Dar es Salaam Maritime Institute
NIT	-	National Institute of Transport
ATCL	-	Air Tanzania Company Limited
TCAA	-	Tanzania Civil Aviation Authority
IATA	-	International Air Transport Association
SITA	-	Societe International Telecommunication Aeronautique
IOSA	-	IATA Operation safety Audit
RAHCO	-	Railway Assets Holding Company
TAA	-	Tanzania Airport Authority
KOJ	-	Kurasini Oil Jet
TANROAD	-	Tanzania Roads Agency
WIM	-	Weigh in Motion Weighbridge

TCRA	-	Tanzania Communication Regulatory Authority
TTMS	-	Telecommunication Traffic Monitoring Systems
TRA	-	Tanzania Revenue Authority
VAT	-	Value added tax
GCLA	-	Government Chemistry Labaratory Agency
TAMISEMI	-	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa